**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MKOA WA NJOMBE**
**MTIHANI WA MAANDALIZI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**
**KIDATO CHA SITA- 2024**

**121/1** **KISWAHILI 1**

**MUDA: Saa 3:00** **MACHI 2024**

---

# MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

**SEHEMU A: ( Alama 40).**

1. a) Maana ya maneno : alama **03 @ 0.5**
   i. **Usanifishaj**i ni kitendo cha kuteua lahaja au lugha na kuifanyia marekebisho ili iweze kutumika katika mawasiliano rasmi;
   ii. **Kamati** ni kikundi cha watu waliochaguliwa kutokana na kundi kubwa la watu ili kushughulikia kazi au jambo fulani
   iii. **Sud**i ni bahati
   iv. **Inda** ni kuwa na wivu au husuda
   v. **Hamasa** ni hamu au uwezo wa kufanya jambo kwa bidii
   vi. **Sera** ni mikakati, au mongozo au mipango mbalimbali

(b) Kichwa cha habari ni USANIFISHAJI WA KISWAHILI **(Alama 01)**

(c) Usemi Mungu hamtupi mja wake unamaanisha kila mtu ana riziki yake kutoka kwa mwenyezi Mungu**. (alama 01)**

(d) kufupisha kwa maneno 100.

- Mtahiniwa asome habari yote mpaka aielewe.
- Achague taarifa na maneno muhimu tu (abaini mawazomakuu tu)
- Katika ufupisho wake mtahiniwa azingatie

i. Maana ya kicheko
ii. Faida za kicheko kama vile kuondoa mikunjo ya uso, kuongeza muda wa kuishi, kuondoa upweke
iii. Hasara za kutocheka kama vile maradhi, migogoro.

- Mtahiniwa aandike ufupisho kwa kutumia maneno yake mwenyewe bila kupoteza maana ya msingi
- Kuandika ufupisho kama inavyotakiwa.
- Kuandika ufupisho kwa kuzingatia taratibu za kiuandishi na usahihi wa idadi ya maneno aliyopewa. (**alama 05)**

2. (a) kishazi huru ni aina ya kishazi ambayo hutoa taarifa kamili katika tungo. Mfano mtoto anacheza mpira *alama 02%*

(b)Mtahiniwa anatakiwa ajibu swali hili kwa kuonesha miundo mitatu ya kishazi huru.

i. Kitenzi kikuu peke yake.
   **mfano**
   Juma alicheza
   Sisi Tutalima
   Watoto Wanakula

ii. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu
   **Mfano;**
   Mwajuma alikuwa anafundisha
   Motto atakuwa amelala

iii. kitenzi kishirikishi na nomino na au kivumishi.
   **mfano**
   Dani ni mtoto mzuri
   Ile ni nchi kubwa
   Swala ndiye mnyama mkorofi

**Alama 06 @02.**

3. Mtahiniwa anatakiwa kujibu swali hili kwa kuonesha mbinu za kuondoa utata katika matumizi ya lugha**. (hoja tano**).
   i. Kufafanua maneno au tungo zenye maana zaidi ya moja
   ii. Kutumia alama za uandishi kwa usahihi
   **Mfano** ; mkato,nukta, swali, kushangaa n.k
   iii. Kutumia maneno kwa kuzingatia muktadha na hadhira.
   iv. Kuzingatia upatabnisho wa kisarufi.
   v. Kuzingatia matumizi ya kiambishi au kiwakilishi na si kiambata ndani ya tendo kinachojulisha nomino fulani ni shamirisho katika tungo hiyo.
   **Mfano ;**
   - Ameua chui ( chui ni chamirisho). Pakiwa na utata utatajwa mtenda katika kiima. **10 @ 02.**

   vi.Kuepuka matumizi ya lugha ya kifasihi.

4. Mtahiniwa anatakiwa kujibu swali hili kwa kuonesha maumbo matano yanayodhihirisha utokeaji wa mofu ya kauli ya utendeshi au usababishi na kwa kila mofu aoneshe mfano mmoja..
   i. –esh—

Mfano

Bibi alimbebesha mzigi mtoto wake

ii. –ish—

Mfano ; Juma alipitisha kamba kwenye mti.

iii. _lish_

Mfano

Joshua alimkarisha mtoto

iv. _lesh_

Mfano;

Kiongozi amemzolesha Doto uchafu.

v. _fy_

Mfano;

Matukio mengi yanaogofya

vi. _Z_

Mfano;

Shangazi alimwoza mtoto wake

**10 @ 02**

**SEHEMU B (Alama 60)**

5. Mtahiniwa anatakiwa ajibu swali hili kwa kuzingatia mambo ya msingi katika uandishi wa barua rasmi au kikazi kama vile;
    i. Anwani ya mwandishi ( 02)
    ii. Tarehe (01)
    iii. Anwani ya mwandikiwa (02)
    iv. Mwanzo wa barua (01)
    v. Kichwa cha barua (02)
    vi. Kiini cha barua (08)
    vii. Mwisho wa barua 01)
    viii. Saini ya mwandishi (01)
    ix. Jina la mwandishi (01)
    x. Cheo cha mwandishi (01)

6. Mtahiniwa anatakiwa kujibu swali hili kwa kuzingatia yafuatayo ;

**Utangulizi**: Mtahiniwa anatakiwa kutoa maana ya lahaja, pia kwa ufupi aoneshe sababu zilizopelekea lahaja ya kiunguja kusanifiswa. (alama 03).

**Kiini** : Mtahiniwa anatakiwa kutoa hoja tano zinazoonesha sababu zilizochangia kudumaa kwa lahaja nyingine mara baada ya lahaja ya kiunguja kuteuliwa na kusanifishwa. Sababu hizo ni kama ;
    i. Matumizi ya lahaja ya kiunguja katika vyombo vya habari
    ii. Kutumiwa katika masuala ya sayansi na kiteknolojia
    iii. Hadithi ya lahaja ya kiunguja
    iv. Kutumiwa katika shughuli zote za mawasiliano

v. Wingi wa watu
vi. Kuandikwa kwa kamusi za lahaja ya kiunguja.
**Hoja tano** zingine zinazoendana na hizi (na nyingine zinazoendana nazo) @ **alama 03=15.**
Hitimisho : mtahiniwa anaweza akahitimisha kwa kuonesha umuhimu wa usanifishaji. **(alama 02).**

7. Mtahiniwa anatakiwa kujibu swali kwa kuzingatia ;
**Utangulizi** : Mtahiniwa anatakiwa kutoa maana ya kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili. Pia aoneshe mambo yaliyopelekea lugha kukua na kuenea kipindi cha utawala wa waingereza nchini tanzania. **(alama 03).**
Kiiini : mtahiniwa anatakiwa aoneshe namna waingereza walivyodumaza kiswahili nchini Tanzania**.**
   - Mtahiniwa atoe hoja tano **(05)**

i. Wakati wa usanifishaji wa lugha ya kiswahili hawakuwahusisha wazalendo.
ii. Katika shughuli za kiutawala kiswahili kilihitajika tu kwa ajili ya ajira katika ngazi za chini za utumishi.
iii. Katika elimu, kiswahili kilitumika kufundishia elimu ya msingi na kwenye vyuo vya walimu wa shule za msingi.
iv. Vitabu vilivyotolewa na wakoloni wa kiingereza vilikuwa na makosa mengi sana ya kisarufi hivyo kudumaza sarufi ya kiswahili.
v. Kuondolewa kwa kiswahili kwenye mfumo wa elimu na kutoendelezwa kisarufi miaka ya 1950-1960 kulikwamisha maendeleo ya kiswahili nchini Tanzania.
vi. Kasumba za wasomi wa Kitanzania (**hoja tano ( 05) @ 03=15**
Hitimisho;
Mtahiniwa aoneshe hitimisho linaloendana na hitaji la swali. (**alama 02)**

8. Mtahiniwa anatakiwa kujibu swali hili kwa kuzingatia:
**Utangulizi**: mtahiniwa atoe fasili ya tafsiri pia aoneshe aina mbalimbali za tafsiri (**Alama 03)**
Kiini; mtahiniwa anatakiwa aoneshe umuhimu wa taaluma ya tafsiri katika maisha ya kila siku ya binadamu;

i. Chombo cha mawasiliano
ii. Chombo cha kueneza utamaduni
iii. Chombo cha kujifunzia na kufundishia lugha
iv. Kiliwazo cha nafsi ya mfasiri
v. Husaidia kuziba mapengo ya kimsamiati au kimaana baina ya lugha
vi. Tafsiri ni kama kitega uchumi
Ataj**e hoja (05) @ 03 =15**
Hitimisho: mtahiniwa atoe maelezo mauri ya kufunga hoja zake katika mpangilio wenye mantiki (**alama 02).**